BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI

Kikao cha Sita – Tarehe 22 Februari, 2023
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Mwenyekiti wa Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo:

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo ya mwaka 2022/2023.

## II. MASWALI:

Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

170. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Naipongeza Serikali kwa kutenga kiasi cha fedha za mkopo wa UVIKO 19 ili kuwawezesha wajasiriamali.

(a) Je, ni wajasiriamali wangapi wanawake waliofaidika na mkopo huu.

(b) Je, ni kiasi gani mpaka sasa kilichotumika kuwapatia wananchi mkopo huo.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

57. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Zanzibar kwa nafasi na mjengeko wake, ina sababu kubwa ya kulishughulikia suala zima la utayari na udhibiti wa maafa kwa lengo la kujikinga, kukabiliana na kujenga ustahamilivu na masuala ya maafa. Kwa bahati mbaya, pamoja na kuunda Kamisheni ya Kujikinga na Maafa, bado suala zima la kujikinga na maafa linakabiliwa na changamoto mbali mbali:

(a) Je, Serikali haioni haja ya kufanya mabadiliko ya kisera, kitaasisi na kisheria ili suala la maafa liwe sehemu ya miamala na mienendo yetu.

(b) Je, Serikali haioni haja ya Kikosi cha KMKM kufanyiwa marekebisho ili badala ya kujihusisha zaidi na kuzuia magendo, ijikite pia katika masuala ya usalama na kukabiliana na maafa katika nchi yetu.

(c) Je, Serikali ina mpango gani bora wa kuvijengea uwezo wa kimafunzo na kuvipatia vifaa vya kisasa vikosi vya KMKM (Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo) na KZU (Kikosi cha Zimamoto na Uokozi) ili kukabiliana na maafa.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

158. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kulipa kodi ni jambo la lazima kwa maslahi mapana ya kukuza uchumi na utoaji wa huduma bora kwa wananchi

(a) Je, ni asilimia ngapi ya wananchi ambao hawakusajiliwa rasmi katika mfumo wa kulipa kodi.

(b) Je, Wizara inachukua mikakati gani ya kuhakikisha inawafikia wale wote ambao hawakusajiliwa katika mfumo rasmi wa kulipa kodi.

(c) Ni mifumo ipi mbadala itakayowajenga imani wananchi kwamba kulipa kodi kwa hiari ni kitendo cha uzalendo na kuipenda nchi yao ili kukuza uchumi wao.

Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

145. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kwa kuwa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo hupata fursa ya kushiriki vikao mbali mbali vya mashirikiano baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

(a) Je, Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki imefanya jitihada gani za kukuza lugha ya Kiswahili.

(b) Je, hatua gani za kidiplomasia zimefikiwa za kukifanya Kiswahili kuwa lugha rasmi ya Umoja wa Afrika (A.U) na Umoja wa Mataifa (UN).

(c) Je, ni idhaa gani za redio za Kimataifa zilizoongezeka katika kipindi cha miaka ya karibuni katika kutumia lugha ya Kiswahili kwenye matangazo yao ukiacha zile maarufu kama BBC, DW, VOA, CFI, Radio China Kimataifa na Redio Iran.

Wizara ya Afya:

119. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Wananchi na Wafadhili mbali mbali wamekipatia Kituo cha Afya cha S.O.S, vifaa na vitendea kazi vya kisasa pamoja na vipimo vya magonjwa tofauti, lakini kwa bahati mbaya sana kuna ukosefu wa wataalamu wa kuvitumia vifaa hivyo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia wataalamu watakaoweza kuvitumia vifaa hivyo katika kituo cha S.O.S.

Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

108. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Wazanzibari walijawa na matumaini makubwa kwamba iko siku nao nchi yao itakuwa ni miongoni mwa nchi ambazo zinaweza kutoa mafuta na gesi duniani kutokana na tafiti mbali mbali zilizofanywa hapo awali na hivi karibuni, lakini kutokana na ukimya uliokithiri unawapelekea Wazanzibari hao kuyapoteza matumaini yao hayo.

(a) Je, ni hatua gani zimefikiwa hadi sasa juu ya suala hili la mafuta na gesi.

(b) Je, ukweli hasa ni upi juu ya ukimya uliokithiri kuhusiana na suala hili.

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:**

51. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

Ustawi bora wa watoto ndio uhai wa taifa letu. Hali ya maisha ya watoto imeendelea kukosa mwanga na kukumbwa na matatizo mengi kabla ya kufikia miaka 18. Ripoti ya UNICEF ya 2017/2018 inaonesha kuwa, mtoto mmoja wa kike kati ya ishirini, ameripoti japo tukio moja la unyanyasaji wa kijinsia kabla ya kufikia miaka 18. Aidha, mtoto mmoja kati ya watoto 10 wa kiume ameripoti angalau tukio moja la unyanyasaji wa kijinsia.

(a) Je, ni ipi takwimu ya Zanzibar kwa miaka mitano iliyopita (2017-2022) kuhusiana na unyanyasaji wa kijisia.

(b) Je, Serikali inashirikiana vipi na Jumuiya za Kimataifa kama vile UNICEF katika kupambana na changamoto tofauti zinazohusiana na masuala ya unyanyasaji wa kijinsia kwa watoto.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

64. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Ili Sekta ya Kilimo ilete ufanisi na tija kubwa kwa wakulima hususan wakulima wadogo wadogo, inahitaji uwepo wa viwanda vyenye mnasaba na uzalishaji wa Sekta ya Kilimo.

(a) Je, tuna viwanda vingapi ambavyo vinazalisha bidhaa zinazotokana na uzalishaji wetu kwenye Sekta ya Kilimo.

(b) Ni upi mkakati wa Serikali katika kuhamasisha viwanda vyenye kuzalisha bidhaa za kilimo nchini mwetu.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

9. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

   Bandari ya Malindi hutoa huduma maridhawa kwa wanachi wote waliopo katika kisiwa cha Unguja, kwa maana ya wote wanaoishi katika Mikoa ya Kaskazini na Kusini Unguja bila usumbufu wa aina yoyote.

   Je, ni lini Serikali itajenga bandari kama ya Unguja katika eneo la mji wa Chake Chake katikati ya kisiwa cha Pemba, ili kupunguza usumbufu wa masafa marefu kwa wasafiri wanaotoka Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa ajili ya kufuata bandari iliyoko Mkoani.

60. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

   Hatuwezi kwenda sambamba na kasi ya maendeleo ya teknolojia duniani, bila ya kuekeza zaidi kwenye Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Information and Communication Technology (ICT)) na ubunifu.

   Je, Wizara yako inawaandaa vipi vijana wanaojikita kwenye tasnia ya ubunifu wa vitu mbali mbali vyenye manufaa kwa jamii.

79. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

   Katika bandari ya Zanzibar kuna mashine tatu za ukaguzi kwa kila kitengo cha mji salama ambazo ni mbovu kwa muda mrefu sasa, jambo ambalo linasababisha msongomano mkubwa wa abiria.

   Je, ni lini mashine hizo zitatengenezwa ili kuepusha msongomano wa abiria hasa kipindi cha mapumziko ya wanafunzi.

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

69. MHESHIMIWA SALMA MUSSA BILAL (Nafasi za Wanawake): Namuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kuna kila sababu ya kuunga mkono nia njema ya Wizara yako ya kuwasaidia wananchi katika kilimo cha "Green House" kutokana na kilimo hicho kutoa faida kubwa licha ya gharama kubwa ya matayarisho yake.

(a) Kwa nini Wizara yako inashindwa kuandaa mpango kazi wa kuelimisha wananchi juu ya kilimo hiki pamoja na kuwawezesha katika hatua za awali.

(b) Ni mara ngapi Wizara imekuwa ikijaribu kufikisha huduma hizi za kilimo vijijini na kushindwa kutekelezeka.

(c) Je, Serikali imejipanga vipi kutafuta nyenzo za kisasa kwa ajili ya kilimo hiki ambazo watapelekewa wananchi hao wanyonge.

Wizara ya Maji, Nishati na Madini:

92. MHESHIMIWA BAHATI KHAMIS KOMBO (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Pamoja na juhudi zinazochukuliwa na Serikali yetu katika kuhakikisha wananchi wetu wanapata huduma ya maji safi na salama, kumeendelea kujitokeza kwa kiwango kikubwa tatizo la kukosekana kwa huduma hiyo ikiwa ni pamoja na shehia ya Mgagadu.

Je, ni lini tatizo hili la maji litamalizika katika shehia hiyo.

III. HOJA ZA KAMATI:

Mwenyekiti wa Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo:

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo ya mwaka 2022/2023.

**Zanzibar,**
**22 Februari, 2023.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**